

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SIMU YA UPEPO: "REGCOM"

SIMU NA: 023-220-2098

FAX NA. 023-220-2502

E-mail: raslindi@tamisemi.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA,

S.L.P. 1054,

LINDI.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Mhe. Godfrey Zambi na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Mhe. Halima Dendego wanawajulisha wataanzania wote kuwa Maonesho ya Nanenane Kitaifa kwa mwaka 2017 yatafanyika Kanda ya Kusini kwenye Viwanja vya Ngongo – Manispaa ya Lindi kama Mkoa ulivyopokea barua kutoka Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika yenye Kumb. Na. EA.18/45/01/121 ya tarehe 10 Februari, 2017.

Maandalizi ya maonesho haya yanaendelea kwa kila mdau/mshiriki kuendelea kuboresha maeneo yake. Aidha, wadau wote ambao ni Wakuu wa Taasisi za serikali na binafsi, Wafanyabiashara, Viongozi wa Dini, Viongozi wa Vyama vya Siasa, Wanahabari na wadau wengine wa maonesho wa Kanda ya Kusini wanasisitizwa kuhakikisha wanashiriki katika kikao cha wadau kitakachofanyika tarehe 12/04/2017 katika Viwanja vya Ngongo kwenye ukumbi wa Naliendele saa tatu asubuhi.

Kauli Mbiu ya Maonesho ya Nanenane mwaka huu mtaarifiwa pale itakapokuwa tayari.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Elibariki J. Mafole'.

Elibariki J. Mafole

Afisa Habari

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi.

01 April, 2017